Matendo Haramu Husiani ya Watu Binafsi na Mashirika Yaliyoorodheshwa ya Korea Kaskazini

Imetayarishwa na Shawna Meister

1.1 UTANGULIZI

Watu binafsi na mashirika yanayokiuka vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) pia mara nyingi huwa yanatekeleza ukiukaji madhubuti wa sheria na kanuni za nchi. Shughuli za usambazaji zinazotekelezwa na watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa ya Jamhuti ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo (DPRK) zinaweza kuwa na madhara, miongoni mwa mengine, kwa usalama wa nchi wa taifa, uadilifu wa taasisi za fedha za nchi, kanuni za uuzaji nje, au udhibiti wa mipaka. Kwa mfano, usafirishaji wa nyenzo au bidhaa zozote zilizowekewa vikwazo mara nyingi huwa zinhitaji kauli bandia za mamlaka za ushuru, kwa kutoa hati bandia, au kutoa hongo kwa maajenti wa mipaka. Matendo haramu husiani pia yanaweza kuhusishwa na hatari za ziada kwa nchi, kama vile mpito haramu wa nyenzo hatari zinazohatarisha afya na usalama wa yoyote anayeshughulikia usafirishaji huu, au ambazo, kunapotokea ajali, zinaweza kusababisha maafa mengi yaliyosambaa ya binadamu. Ingawa nci zinafanya juhudi ili kujilinda dhidi ya ukiukaji uwezekanao wa sheria zao wenyewe, inaweza kuwa taabu kwa nchi kutambua shughuli husiani zinazofanywa na watu binafsi na mashirika yanayoorodheshwa. Muhtasari huu utasaidia kufafanua ukiukaji haramu au unaovunja kanuni ambao umeonekana au kudokezwa ambao unaweza kuhusishwa na ukiukaji tofauti wa vikwazo.

1.1 MUHTASARI WA MBINU

Kwenye tathmini inayoendelea ya watu binafsi na mashirika yote (k.v., kampuni, mashirika, mawakala n.k.) yaliyoorodheshwa kwenye mfumo wa vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini, sababu na matendo ya kiini ya kuorodheshwa kwao yalikaguliwa. Yanapopatikana, maelezo ya kuunga mkono uorodheshaji huu yalikusanywa na kuchambuliwa, na ufahamu wowote ulioweza kupatikana kwa kutokuwepo maelezo ya ziada ya tabia ya kihalifu au ukiukaji wa kikanuni yalifanywa.[1] Kila ukiukaji ulipewa

[1] Rejelea orodha ya Vikwazo Vilivyojumuishwa vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ya watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa kwenye mfumo wa Korea Kaskazini (zilizoorodheshwa kama KPi na KPe kwenye hati) hapa:

Rico Carisch
rico.carisch@comcapint.com
+1-610-390-9541

www.comcapint.com
110 West 94 Street – 2D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
loraine.rickard-martin@comcapint.com
+1-917-715-2142

alama kulingana na ubora wa unaouunga mkono, huku alama kubwa zikiwemo maelezo ya Umoja wa Mataifa na maelezo ya kutoka nje ambayo yanaaminika (k.v., ripoti za kuaminika za vyom bo vya habari). Data hii kisha ilichambuliwa ili kupata ruwaza, kama vile ukiukaji unaofanyika mara kwa mara, sifa za pamoja, maelezo madhubuti na dhaifu, n.k., na pia mazingatio ya kipekee au yanayoweza kuwa muhimu. Matokeo kwenye utafiti huu wa kifani yanawakilisha sampuli ya data iliyochukuliwa kuwa ni maelezo muhimu kuhusu ukiukaji kulingana na ripoti za Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ambayo inamaanisha kuwa ruwaza zilizoripotiwa ni za kuaminika sana.

1.1.1 WATU BINAFSI

Ni taabu kung'amua ruwaza husiani za kihalifu za watu binafsi walioorodheshwa wa Korea Kaksazini kwa ajili ya maelezo machache yanayopatikana kwenye hati za Umoja wa Mataifa kuhusu matendo maalum ambayo yanaonekana kuwa yanawezesha ukiukaji. Lisilowiana na haya ni ithibati ambayo inadokezwa mara nyingi kwenye ripoti za wataalamu wa Umoja wa Mataifa ya mworodheshwa kufanyia kazi au kufanya kazi na mashirika yaliyoorodheshwa. Licha ya haya, tathmini ya matendo ya watu binafsi ambao maelezo ya ziada ya Umoja wa Mataifa yapo inaonyesha ushara za matendo husiani ya kihalifu yanayohusu usafiri, hadhi za kidiplomasia, miamala ya fedha, marufuku ya silaha, biashara na matendo ya wafanyakazi.

Ukiukaji wa vikwazo unaoonekana sana unatokea wakati watu binafsi walioorodheshwa wanasafiri au kuishi nje ya Korea Kaskazini. Watu wote walioorodheshwa wamewekewa makatazo ya usafiri na ukwamishaji mali, ambayo inamaanisha kuwa hawafai kuishi kwenye nchi ambayo si Korea Kaskazini, hawafai kuvuka mipaka ya kimataifa, wala hawafai kufikia rasilimali za fedha. Hata hivyo, watu binafsi kadhaa walioorodheshwa wamepatikana kuwa wamesafiri, au wameshukiwa kuwa wamesafiri, kupitia au hadi kwenye nchi zingine, huku wengine wanaishi kwenye nchi zingine.[2] Orodha Iliyojumuishwa ya Vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa inaashiria kuwa wachache kati ya watu hawa wanatumia lakabu anuwai au pasipoti kadhaa,[3] ambayo inamaanisha kuwa watu hawa, na kuna uwezekano ni wengi zaidi, wanazalisha au wanatumia hati bandia za usafir. Pasipoti bandia zinatolewa na viongozi wa Korea Kaskazini zikiwa na majina yaliyobadilishwa kimakusudi na maelezo mengine yanayotambulisha au yanabadilisha kiharamu na wahusika wengine. Kwenye hali hii au ile, matumizi ya hati kama hizi yanakiuka sheria za kitaifa na kimataifa zinapotumiwa kw lengo lolote, lakini kimahususi ili kupitia kwenye mipaka ya kimataifa.

---

https://www.un.org/securitycouncil/content/un-sc-consolidated-list. Maumbizo anuwai yanapatikana.

[2] Kwa mfano tazama watu binafsi wa 1, 8, 14, 16-21, 24, 27, 30, 31, 33, 34, 46, 52, 56, 59, 61, 62, 67–75, 77, na 78.

[3] Watu binafsi walioorodheshwa wa 18, 21, na 30 ni baadhi ya mifano.

Baadhi ya watu wenye uraia wa Korea Kaskazini au wanaofanya kazi kwa niaba ya miradi ya usambazaji ya Korea Kaskazini bado wanaweza kusafiri licha ya kuwa wanaonekana kuwa hawatumii hatua za kulaghai.[4] Uwezo wa kuingia au kupita kwenye nchi zingine unawezekana tu ikiwa nchi ina ukosefu wa teknolojia ya mipaka, miundombinu, au uwezo wa kutambua walioorodheshwa. Kwa kuzingatia idadi ya walioorodheshwa (80 wakati wa muhtasari huu), na kuwa watu binafsi wanasafiri kwenye nchini zenye mfululizo tofauti wa uwezo wa mipakani, kuna uwezekano mkubwa kuwa baadhi ya walioorodheshwa wa Korea Kaskazini wanawapatia hongo maafisa wa mipaka.

Watu binafsi wanaotumia makaratasi bandia ya kujitambulisha au wanaohinga maafisa wa nje mara nyingi pia huwa wanatumia mikakati ya kihalifu kwenye juhudi zao zingine. Wakiwa ng'ambo, wanaweza kupata nyumba, benki, mawasilianoanga, na usafiri nchini, au huduma za kimataifa za kusafirisha mizigo – zote kupitia mtumizi ya utambulisho bandia na kutumia hongo, na kwa kukiuka sheria na kanuni za kitaifa.

Maombo mengine ya kuzingatiwa kutoka kwenye uchambuzi wa matendo husiani ni matumizi mabaya ya hadhi za kidiplomasia yanayofanywa na baadhi ya mabalozi wa Korea Kaskazinina maafisa wa wizara wanapokuwa wanatenda shughuli kwenye nchi zingine.[5] Chini ya Maafikiano ya Vienna ya Uhusiano wa Kidiplomasia, wanadiplomasia na wawakilishi wengine wa serikali walipewa cheti rasmi wafanye shughuli kwenye nchi nyingine, wana kinga takriban kamili dhidi ya kufunguliwa mashtaka ya kihalifu kwenye nchi inayokaribisha.[6] Hii haiwaondolei jukumu la kutii sheria na kanuni za nchi inayopeana cheti. Licha ya hayo, baadhi ya wafanyakazi wa kidiplomasia walioorodheshwa wametumia hadhi yao ili kukiuka vikwazo vya Umoja wa Mataifa kwa kufanya miamala ya fedha kwa niaba ya mashirika yaliyoorodheshwa, kutafuta na kununua nyenzo za usambazaji, au kufanya biashara ya bidhaa zilizowekew marufuku kama vile silaha na nyenzo husika.[7] Wengine wameshikwa wakisafirisha kiasi kikubwa cha pesa au dhahabu ambayo inaenda kinyume na vikwazo vya Umoja wa Mataifa na majukumu ya kitaifa ya kuripoti ulanguzi wa pesa, na pia kuepuka ripoti za miamala ya fedha inayoshukiwa kwa kitengo cha taifa cha upelelezi wa fedha.[8] Mbali na kukiuka vikwazo na maafikiano ya kimataifa huku wakiwepo au wakifanya shughuli kwenye nchini zingine zhini ya hadhi ya kidiplomasia, shughuli za walioorodheshwa zinaweza kujumuisha kuvunja baadhi ya sheria au kanuni za nchi. Kwa mfano, miamala haramu

[4] Kwa mfano, tazama watu binafsi wa 31 na 33.

[5] Kwa mfano, tazama watu binafsi walioorodheshwa wa 1, 14, 21, 29, 33, 34, 36, na 44.

[6] Umoja wa Mataifa. *Maafikiano ya Vienna ya Uhusiano wa Kidiplomasia (Mkataba wa 1961)*. Vienna: Austria. (2005): Vifungu vya 31 na 41(1).

[7] Kwa mfano, tazama watu binafsi walioorodheshwa wa 14, 21 na 29.

[8] Kwa mfano, tazama watu binafsi walioorodheshwa wa 30 na 35.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

ya fedha na biashara ya silaha na nyenzo zingine huku wakifanya kazi kwenye nyadhifa rasmi za kidiplomasia za Kore Kaskazini zimetekelezwa na wanadiplomasia walioorodheshwa na ambao hawajaorodheshwa wa Korea Kaskazini.[9]

Aina zingine za ukiukaji wa vikwazo, kama vile ukiukaji wa ukwamishaji mali, marufuku ya silaha, kupinga usambazaji, au vikwazo vya biashara pia mara nyingi zinazhusishwa na matendo husika yaliyo haramu. Watu binafsi walioorodheshwa ukwamishaji mali wa Umoja wa Mataifa na vikwazo vingine vya fedha pia huwa maranyingi wanajihusisha na shughuli husika za kihalifu, kama vile kuunda hati bandia, kufanya ulanguzi wa pesa, au kuunda au kutumia kampuni zifichazo, kwa malengo ambayo hayajaidhinishwa na msajili wa kampuni wa nchi inayokaribisha.[10] Kwa mfano, baadhi ya watu walioorodheshwa wanaowakilisha benki za Korea Kaskazini au kampuni za biashara nchini Uchina, wameunda kampuni zifichazo na wamefanya miamala mikubwa ya fedha kwa niaba ya Korea Kaskazini.[11]

Watu binafsi walioorodheshwa watapuuza kanuni za biashara ya uuzaji nje au kuzivunja nguvu kwa kauli za uwongo. Ufikishaji wa bidhaa za kijeshi kutoka Korea Kaskazini hadi nchi zisizokuwa imara au zenye vita unaweza kuishia mikononi mwa wapiganaji, na kuvunja nguvu juhudi za upatanishi na kuchangia vurugu zaidi au kusaidia ukiukaji wa haki za binadamu kwa njia isiyokuwa moja kwa moja.[12] Baadhi ya maafisa wa Korea Kaskazini wanaweza kuwa wanajihusisha na shughuli za ziada za kiovu ambazo zinadhuru nchi zinazowakaribisha; kwani, angalau mtu mmoja binafsi amewekewa vikwazo kwa ajili ya kufanya ujasusi.[13]

Baadhi ya watu binafsi walioorodheshwa pia wametambuliwa kuwa wanaongoza na kusimamia vikundi vya wafanyakazi wa Korea Kaskazini. Kwenye hali hizi, walioorodheshwa watakuwa si tu wanachangia kukiuka katazo vikwazo vya Umoja wa Mataifa dhidi ya matumizi ya wafanyakazi ili kuizalishia pesa Korea Kaskazini, lakini pia wanaweza kuwa wanachangia ukiukaji wa haki za binadamu na sheria za wafanyakazi. Vikosi rahisi na visivyodhibitiwa vya wafanyakazi wa Korea Kaskazini vinaweza kupunguza viwango vya mishahara vya nchi, vinaweza kuunda viwango vya sekta vyenye upungufu wa usalama, au vinaweza kuongeza vurugu la jumla la wafanyakazi kwenye nchi inayokaribisha. Kwa ziada, kwa sababu mishahara ya wafanyakazi hawa huwa inadhibitiwa na wanadiplomasia wa Korea Kaskazini, miamala mikubwa ya pesa zisizodhibitiwa na huduma kubwa za usafirishaji mizigo zinaweza kutokea kutokana na haya.[14]

---

[9] Tazama watu binafsi wa 1, 14, 21, na 29. Pia tazama paragrafu ya 50 na Nyongeza XVII D na E au UNSC S/2013/337, ripoti ya Jopo la Wataalamu, ili kupata mifano ya wanadiplomasia wa Korea Kaskazini ambao hawajaorodheshwa kusafirisha zana za kijeshi na kutumia akaunti za kidiplomasia ili kuficha miamala ya fedha.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

1.1.2 MASHIRIKA

Maelezo zaidi kuhusiana na ukiukaji wa vikwazo unaofanywa na mashirika yapo, ambayo inaashiria uwezekano ulioongezeka wa matendo haramu husiani yanayoweza kuathiri vibaya nchi wanachama za Umoja wa Mataifa na yanayoweza kukiuka sheria na kanuni za nchi. Kama vile watu binafsi, mashirika yaliyoorodheshwa yanafanya ukiukaji kuhusiana na hadhi ya kidiplomasia na aina ya shughuli. Kwa mfano, baadhi ya balozi zimeorodheshwa kama anwani ya kuendesha shughulikwa baadhi ya mashirika yaliyoorodheshwa. Haya mara nyingi huwa ni mashirikisho ya kampuni za serikali za Korea Kaskazini ambayo yanaweza kufanya shughuli kadhaa: kama maajenti wa kibiashara wa sekta ya uuzaji nje wa silaha inayoendelea kukua ya Korea Kaskazini, kama wanunuzi wa bidhaa na nyenzo za kijeshi zisizoruhusiwa ili zisafirishwe hadi nchini Korea Kaskazini, au kama wakandarasi wa jumla wa mashirika mengine ya Korea Kaskazini ambayo yanafikisha huduma za ujenzi na huduma zingine kwa nchi hiyo.[15]

Mfano maarufu zaidi wa mashirikisho haya ni Shirika la Biashara za Kuendeleza Uchimbaji Madini la Korea (KOMID), iliyoorodheshwa mnamo 2009, ambayo inatekeleza uingizaji nchini/uuzaji nje wa silaha za kawaida, nyenzo za usambazaji zinazohusu makombora ya mbali, na kutoa huduma za jumla za kandarasi kwa miradi ya ujenzi wa kiraia na kijeshi. KOMID imetumia mapochi ya kidiplomasia yaliyofungwa ili kuficha hati za usafirishaji ili kuzuia yaliyomo kwenye mzigo yasijulikane.[16] Kwa kuzingtia yale yanayojulikana kuhusu KOMID, mashirikisho ya Korea Kaskazini yanayofanya shughuli nyuma ya kinga ya kidiplomasia yanaweza kufanya biashara ya silaha au nyenzo za usambazaji kinyuma na sheria kwa kuvuka mipaka ya kimataifa au kupitia kwenye nchi zingine, na kukiuka sheria na kanuni zingine za nchi na kanuni za kimataifa za usalama wa usafiri. Kama watu binafsi, shughuli za mashirika zinazotumia hadhi ya kidiplomasia zinakiuka sheria na kanuni za nchi na zinapunguza uadilifu na heshima ya maingiliano ya mara kwa mara ya kidiplomasia.

Pia, kama watu binafasi, mashirika yanayofanya aina fulani za kazi pia yana uwezekano mkubwa wa kufanya matendo haramu kisheria au ukiukaji wa kanuni kwenye nchi zingine. Mashirika kadhaa yanafanya matendo kama kampuni zifichazo mashirika mengine au zinatumia lakabu.[17] Ili kufanya shughuli zao, baadhi ya mashirika

[10] Kwa mfano, tazama watu binafsi wa 35 na 77.
[11] Tazama watu binafsi walioorodheshwa wa 35 na 77.
[12] Kwa mfano, tazama watu binafsi wa 27, 31, na 56.
[13] Tazama mtu binafsi wa 40.
[14] Kwa mfano, tazama mtu binafsi wa 30.
[15] Kwa mfano, tazama mashirika ya 1, 3, 16, au 44.
[16] Tazama UNSC S/2018/171, ukurasa wa 132.
[17] Kwa mfano, tazama mashirika ya 1, 2, 3, 5, 7, 13, na 16.

yanajulikana kuwa yanaunda hati bandia, yanasafirisha fedha kiharamu, yanatumia lakabu, yanatumia vituo haramu ili kufanya miamala ya fedha, na labda pia yanahonga maafisa nchini ili kutekeleza shughuli zao. Baadhi ya mashirika yanayofanya shughuli kwenye nchi zisizokuwa imara au zenye vita yanatoa mafunzo ya kijeshi, silaha, na nyenzo, ambazo zinaweza kuchangia kwenye ukiukaji wa haki za binadamu kwenye nchi hizi au zinaweza kuzidi kuharibu amani kwenye maeneo hayo.[18]

Nchi zinazotumia huduma za Korea Kaskazini pia zinaweza kuhusika kwenye ukiukaji wa haki za binadamu za kimataifa au itifaki za kimataifa za wafanyakazi ikipatikana kuwa kampuni hizi za Korea Kaskazini zinalazimu wananchi wa Korea Kaskazini kufanya kazi kwa lazima. Maazimio ya Umoja wa Mataifa ya 2375 na 2397 yanakataza idhini za kufanya kazi kwa raia wa Korea Kaskazini na yanalazimu mataifa yawarudishe kwao wafanyakazi ambao tayari walikuwa wanafaidika na idhini kama hizi za kufanya kazi. Licha ya hayo, miradi inayosimamiwa na kufadhiliwa na Korea Kaskazini inaendelea kwenye nchi nyingi zenye wafanyakazi wa Korea Kaskazini badili ya wafanyakazi wao wenyewe.[19] Kwa ajili mbinu hii ya kukwepa vikwazo inatumiwa kuzalisha mapato kwa serikali ya Korea Kaskazini, kuna uwezekano mkubwa kuwa wafanya kazi wa Korea Kaskazini wanalipwa kidogo, hawapokei chakula, makao, au uangalizi wa kimatibabu wa kustosha, na pia huwa wananyanyaswa kuhusiana kwa kukiuka sheria za wafanyakazi. Kwa ziada, shughuli hii mara nyingi huwa inaondoa mapato kutoka nchi inayowakaribisha kwani wafanyakazi ambao ni wananchi wanaotii sheria hawatumiwi, na kwa hivyo, hawatolipa kodi ya mapato. Athari ya chini zaidi ya kuingiza wafanyakazi wa Korea Kaskazini waliotishiwa ni kuwa itapunguza mishahara ya wananchi. Wafanyakazi wa Korea Kaskazini na raia wengine pia wamepatikana kuwa wanasafirisha kiharamu pesa nyingi sana kutoka nchi zinazochukua wafanyakazi hawa hadi Korea Kaksazini. Mbali na kukiuka vikwazo vya Umoja wa Mataif, uhamishaji huu unakiuka sheria za baadhi ya nchi ambazo zinaweka vikomo vya kiasi cha pesa kinachoweza kuingizwa na kutolewa kwenye cnhi, na unaathiri vibaya majukumu ya kitaifa na kimataifa ya kuripoti ulanguzi wa pesa.[20]

Mashirika yaliyoorodheshwa kwa ajili ya ununuzi au uuzaji wa nyenzo za usambazaji huenda yakawa yanakiuka sheria anuwai za nchi na kanuni za usalama ikiwa bidhaa zitapitia au zitaishia kwenye nchi mwanachama. Kwa mfano, baadhi ya mashirika yanajulikana kuwa yanasafirisha nyenzo hatari mno,[21] kama vile yuraniamu

[18] Kwa mfano, mashirika ya 1, 14, 17, na 21 yanafanya shughuli nchini Siria na Sudani.

[19] Kwa mfano, tazama shirika la 50, Kundi la Kampuni la Miradi ya Nje ya Mansudae, inayofanya shughuli zake kwenye nchi 15 au zaidi, mara nyingi kwa kutumia wafanyakazi wa Korea Kaskazini.

[20] Mansudae, shirika la 50, linajulikana kwa shughuli hii na linafanya shughuli kwenye nchi anuwai ulimwenguni.

[21] Kwa mfano, tazama mashirika ya 4, 39, na 44.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

iliyotakaswa. Kwa mujibu wa taratibu za usimamizi, kuna uwezekano mkubwa kuwa mawakala haya yanaunda hati bandia za nchi, sera za bima, notisi za usafirishaji bidhaa, n.k. kama mbinu moja ya kuficha bidhaa. Ili kufaulu ukaguzi, kuna uwezekano mkubwa kuwa angalau baadhi ya watu binafsi, kama vile wakaguzi wa serikali na maajenti wa mipaka, wanapokea hongo ili kuruhusu upitishaji wa nyenzo hizi. Kwa ziada, kwa ajili ya asili ya kisiri ya kusafirisha bidhaa haramu, huenda mashirika yasijihadhari vilivyo, yasifuate sheria za kitaifa na kanuni za usalama, au yasitii sheria za Shirika la Kimataifa la Usafiri Angani wa Raia (ICAO) au Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini (IMO) za usafirishaji haramu wa nyenzo hatari.

Wakati wa maandishi haya, mfululizo wa hivi karibuni zaidi wa mashirika yaliyoorodheshwa unajumuisha kampuni zinazosimamia au zinazomiliki meli zao wenyewe, au zinazoaminiwa kuwa, zimefanya usafirishaji haramu wa bidhaa kutoka au kuelekea nchini Korea Kaskazini.[22] Ukiukaji huu wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa pia una uwezekano mkubwa kuwa una vunja sheria na kanuni za nchi ambazo bendera yao ilitumiwa na vyombo hivi vya usafiri, na pia kanuni za kitaifa na kimataifa za wafanyakazi na usafirishaji kuhusiana na nyenzo hatari. Vyombo vya usafiri vya Korea Kaskazini, au kampuni za usafirishaji za Korea Kaskazini, mara nyingi huwa zinabadilisha bendera ya vyombo vyao vya usafiri, mara nyingine mara kadhaa, ili kurahisisha uhamishaji haramu wa bidhaa (k.v. makaa ya mawe na mafuta/petroli) au kutekeleza uhamishaji haramu wa bidhaa kutoka meli moja hadi nyingine baharini. Chombo kipya cha usafiri kinasaidia kuficha asili ya makaa ya mawe au petroli kutoka Korea Kaskazini au kituo cha mwisho safarini cha madini mengine ambayo hayaruhusiwi kufikishw nchini Korea Kaskazini kwa mujibu wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa. Hivi karibuni, baadhi ya waendeshaji wa meli za Korea Kaskazini wamejaribu kuepuka kugunduliwa kwa kubwaga mizigo yao ya makaa ya mawe kwenye poti ndogo zilizo mbali, kama vile Kholmsk nchini Urusi, ambapo makaa hayo ya mawe yanaweza kuchanganywa na makaa ya kienyeaji, na muda mfupi baadaye kuchukuliwa na vyombo vipya vya usafiri.[23]

Waendeshaji wa vyombo vya usafiri au kampuni za usafirishaji zinatekeleza ulaghai kadhaa, ambao huenda ni haramu kisheria, kama vile kubadilisha jina la chombo kwa kuonyesha sifa bandia za meli, kama vile nambari za Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini, ujumuishaji wa bima, udumishaji, asili na kituo cha mwisho safarini cha meli.[24] Shughuli hizi zinaweza kuwa zinakiuka sheria za nchi wanachama au zinaahiria matumizi yasiyo ya kwaida ya matendo ambayo hayapendezi kwenye sekta. Baadhi ya mikakati ya ulaghai inahusisha kuzima Mfumo wa Utambulisho wa Kiotomatiki (AIS), ambayo inaficha kuwepo kwake kwa walinzi wa kitaif wa pwani, poti, na mawakala

[22] Kwa mfano, tazama mashirika ya 55-74, kipekee kwa mashirika ya 57, 60, na 71.

[23] Tazama UNSC S/2019/171, ukurasa wa 37.

[24] Kwa mfano, tazama mashirika ya 55 na 74.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

mengine inayofuatilia maji ya bahari ya nchi.[25] Kanuni za kimataifa zinahitaji uendeshaji wa AIS ili kurahisisha huduma za uokozi kwenye hali za dharura.

1.2 MAHOJIANO NA MAPENDEKEZO

Juhudi za usambazaji za Korea Kaskazini hazikiuki vikwazo vya Umoja wa Mataifa tu, bali pia zina athari madhubuti za kisheria na kikanuni kwa mataifa mengi mbayo, kwa ajili ya utata unaohusishwa, mara nyingi huwa yanabakia kuwa hayajulikana na mamlaka husika. Maafisa wa serikali wanafaa kuchukulia kuwa kuwepo kwa mtu binafsi au shirika lililoorodheshwa kwenye vikwazo vya Umoja wa Mataifa, au lenye uhusiano wa karibu na aliyeorodheshwa, kunasababisha hatari kubwa ya hatia za kikanuni na kihalifu. Mapendekezo yafuatayo ni kama miongozo tu na hayafai kufasiriwa kama jibu kamili la usambazaji wa Korea Kaskazini na shughuli zake zingine za kihalifu. Mwitiko mwafaka ni maafisa wote wa serikali kuwa makini zaidi.

1. Maajenti au wananchi wa Korea Kaskazini wanaofanya shughuli kwa niaba ya mradi wa usambazaji wa Korea Kaskazi wanasababisha hatari maalum na za jumla kwa nchi zinazowakarabisha. Kwa sababu ya hatari zaidi inayohusishwa na watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa, serikali zinafaa kuwa makini sana kwenye maingiliano yote ili kuzuia mfululizo mpana wa hatia za kihalifu na kikanuni.

Nchi wanachama pia zinafaa kuchunguza waorodheshwa wa Korea Kaskazini ili kupata shughuli za ukiukaji ziwezekanazo. Hii inaweza kujumuisha ukaguzi wa uhamishaji wa fedha au uchunnguzi wa kina zaidi wa kampuni za Korea Kaskazini, hasi ikiwa balozi zinatumia kwenye vipengele vya taratibu. Mataifa yasiyokuwa imara au yenye vita yanafaa kufuatilia mwendo wa watu binafsi wanaotoka Korea Kaskazini hasa ikiwa wanaonekana kuwa wanafanya shughuli kwenye maeneo vyenye vikundi vilivyojihami.

2. Watu binafsi walioorodheshwa kwenye katazo la usafiri la Umoja wa Mataifa ambao bado wanajaribu kusafiri kimataifa ni ishara ya upungufu uwezekanao kwenye mawakala ya kudhibiti mipaka ya nchi, kwa hivyo, pia ni ishara iwezekanayo ya vitendo vingine haramu vinavyohusu uhamishaji bidhaa mipakani. Mikakati ya ukwepaji wakiukaji inaweza kutokea kutokana na masuala ambayo hayaonekani kuwa ni muhimu, kama kukwepa taratibu za viza ikiwemo ada husika, au kuutumia vibaya mfumo ili kusafirisha silaha kiharamu kwenye vituo vya mipaka vinavyoweza kutumika. Itabidi viongozi wa nchi wazingatie sababu tofauti za kukiuka katazo la usafiri walizo nazo watu binafsi walioorodheshwa. Watu binafsi wanaweza kuwa wanasafiri kwa sababu binafsi

[25] Kwa mfano, tazama mashirika ya 55 na 64.

Viongozi wa nchi wanafaa kutekeleza kikamilifu katazo la usafiri la Umoja wa Mataifa na wahakikishe kuwa mawakala wa mipaka walioko kwenye safu ya mbele wamepewa mafunzo mazuri na wamehamishwa kuhusu vipengele vyote vya usafiri wa watu binafsi walioorodheshwa na Umoja wa Mataifa.

au kwa malengo yasiyokuwa muhimu, au ari ya kusafiri inaweza kuwa na uhusiano na malengo nia za kilaghai zaidi za uhalifu, ambazo, miongoni mwa mengine zinapunguza uwezo wa taifa wa kufuatilia shughuli haramu au shughuli zingine zenye madhara.

3. Baadhi ya watu binafsi na mashirika ya Korea Kaskazini yanatumia hadhi za kidiplomasia ili kutekeleza ukiukaji wa sheria za kimataifa na labda hata sheria za nchi. Kwa kiwango cha chini zaidi, athari kwa mataifa ni upungufu wa uwezo wa kujua shughuli zipi haramu zinatekelezwa ndani ya mipaka yao, huku matokeo makuu yanaweza kujumuisha uingizaji nchini/uuzaji nje wa nyenzo za usambazaji, silaha, au bidhaa zingine zilizowekewa marufuku.

Mataifa yanafaa kupunguza kupeana vyeti kwa wafanyakazi wa kidiplomasia wa Korea Kaskazini, ikiwemo vya kufungua akaunti za benki. Wanadiplomasia ambao lengo na ari yao haiaminiki na ambao wanaonekana kuwa hawashiriki kwenye shughuli za kidiplomasia zilizooidhinishwa wanafaa kuhojiwa na vyeti vyao kukomeshwa kwa kipindi cha muda wa sababu yao rasmi ya kuwepo nchini. Wanadiplomasia wanaokiuka vikwazo vya Umoja wa Mataifa wanafaa kuripotiwa kwa kamati ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Korea Kaskazini, kwa kutii azimio la 1737, na, pindi wanapoorodheshwa kwenye katazo la usafiri la Umoja wa Mataifa, wanaweza kufukuzwa nchini.

4. Mataifa wanaweza kuchukuliwa hatua kwa shughuli za Korea Kaskazini zinazotokea kwenye mataifa yao ambazo zinaweza kukiuka sheria za kimataifa za haki za binadamu na sheria za kimataifa za wafanyakazi yanapokubali vikundi vya wafanyakazi kutoka Korea Kaskazini. Kwa ziada, mataifa yana uwezekano mkubwa wa kupoteza mapato na ukuaji wa uchumi kupungua pale mashirika ya Korea Kaskazini yanapochukua nafasi ya vikosi vya kienyeji vya wafanyakazi.

Mataifa yanafaa kutekeleza sheria ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa vinavyopunguza shughuli za kuzalisha mapato za Korea Kaskazini, kama vile kutoa huduma za ujenzi na huduma zingine, ili kukuza ukuaji wa uchumi wa nchi na kupunguza uwezekano wa ukiukaji wa haki za binadamu na sheria za wafanyakazi usitokee kwenye taifa lao.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

5. Ukwepaji wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Korea Kaskazini kuhusiana na uingizaji nchini na uuzaji nje wa bidhaa zinazouiwa unaweza kuwa na athari mbaya ya moja kwa moja kwa mataifa, hadhi ya sajili zao za usafirishaji, usalama wa vituo vyao vya poti, na ulinzi wa taratibu za kimataifa za usafiri baharini. Ingawa kubadilisha bendera na kubadilisha umiliki, usajili, na bima ya chombo cha usafiri ni shughuli halali, ikiwemo mabadiliko ya mara kwa mara ya kituo cha mwisho cha safari ya meli, mamlaka za kitaifa zinafaa kuwa makini. Mamlaka zinahitaji kujua kuwa matendo kam haya yanaweza kuwa juhudi za kutumia vibaya taifa hilo ambazo zinafanywa na wamiliki au waendeshaji wa meli za Korea Kaskazini ili kuficha matendo yao na zinaweza kuwa sehemu ya muamala wa bidhaa haramu.

Ili kuzuia biashara haramu ya bidhaa na usafirishaji haramu wa Korea Kaskazini, mamlaka za nchi zinafaa kuthibitisha wamiliki na waendeshaji wa vyombo vyote kwa uagalifu sana pale ambapo mamlaka zinashuku kuwa maslahi ya Korea Kaskazini yanaweza kuhusishwa.

Kuna njia nyingi ambapo ukiukaji wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa unatokea pamoja na matendo husiani ya haramu ambayo yanaweza kuenda kinyume na sheria na kanuni za nchi. Athari za matendo haya yanaweza kuhusisha hata hatari za kifedha na kiusalama kwa nchi na raia wake.[26] Nchi zinazotekeleza sheria ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa zinaweza kuchangia kupunguza shughuli za usambazaji na ukiukaji mwingine wenye hatari. Lakini pia zinaweza kupunguza shughuli za kihalifu au shughuli zingine haramu ambazo Korea Kaskazini inafanya bila kujali athari mbaya kwenye nchi husika.

Nyongeza

[26] Matendo haya husiani yamejengwa juu ya msingi wa ripoti za Jopo la Wataalamu na ithibati zingine zinazounga mkono, na kwa hivyo zinaweza kuwa na upungufu wowote uliokuwepo kwenye maelezo ya awali.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Watu Binafsi na Mashirika ya Korea Kaskazini Yanayohusishwa na Matendo Haramu Husiani

Watu Binafsi				
#	**Jina**	**Uhusiano**	**Uraia**	**Tarehe ya Kuorodheshwa**
1	Yun Ho-Jin	Mkurugenzi wa Kampuni ya Biashara ya Namchongang na mkurugenzi wa Kampuni ya Muungano ya Korea Sobaeksu huko Beijing	Korea Kaskazini	7/16/2009
8	Ra Ky'ong-Su	Mwakilishi wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon huko Beijing	Korea Kaskazini	1/22/2013
14	Choe Song Il	Mwakilishi wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon nchini Vietinamu	Korea Kaskazini	3/2/2016
16	Jang Bom So	Mwakilishi wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon nchini Siria	Korea Kaskazini	3/2/2016
17	Jang Yong Son	Mwakilishi wa KOMID nchini Irani	Korea Kaskazini	3/2/2016
18	Jon Myong Guk	Mwakilishi wa ng'ambo wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon	Korea Kaskazini	3/2/2016
19	Kang Mun Kil	Mwakilishi wa ng'ambo wa Shirika la Biashara la Namchongang	Korea Kaskazini	3/2/2016
20	Kang Ryong	Mwakilishi wa KOMID nchini Siria	Korea Kaskazini	3/2/2016
21	Kim Jung Jong	Mwakilishi wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon nchini Vietinamu	Korea Kaskazini	3/2/2016
24	Kim Yong Chol	Mwakilishi wa KOMID nchini Irani	Korea Kaskazini	3/2/2016
27	Ryu Jin	Mwakilishi wa KOMID nchini Siria	Korea Kaskazini	3/2/2016
29	Pak Chun Il	Balozi wa Korea Kaskazini nchini Misri	Korea Kaskazini	11/30/2016

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Watu Binafsi				
#	Jina	Uhusiano	Uraia	Tarehe ya Kuorodheshwa
30	Kim Song Chol	Afisa wa KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016
31	Son Jong Hyok	Afisa wa KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016
33	Ri Won Ho	Afisa wa Wizara ya Usalama wa Nchi ya Korea Kaskazini nchini Siria anayesaidia KOMID.	Korea Kaskazini	11/30/2016
34	Jo Yong Chol	Afisa wa Wizara ya Usalama wa Nchi ya Korea Kaskazini nchini Siria anayesaidia KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016
35	Kim Chol Sam	Mwakilishi wa Benki ya Mikopo ya Daedong (DCB) nchini Malesia, Singapoo	Korea Kaskazini	11/30/2016
36	Kim Sok Chol	Aliyekuwa Balozi huko Burma, Msaidizi wa KOMID	Korea Kaskazini	11/30/2016
40	Cho Il U	Mkurugenzi wa Ofisi ya Tano ya Ofisi ya Jumla ya Upelelezi	Korea Kaskazini	2017-06-02
44	Kim Chol Nam	Rais wa Shirika la Biashara la Korea Kumsan	Korea Kaskazini	2017-06-02
46	Kim Tong-Ho	Mwakilishi wa Banki ya Kibiashara ya Tanchon nchini Vietinamu	Korea Kaskazini	2017-06-02
52	Ri Su Yong	Mwakilishi wa Shirika la Jumla la Ryonbong nchini Kuba	Korea Kaskazini	2017-06-02
56	Jang Song Chol	Mwakilishi wa ng'ambo wa KOMID	Korea Kaskazini	8/5/2017
59	Kang Chol Su	Mwakilishi wa Shirika la Jumla la Ryonbong nchini Uchina	Korea Kaskazini	8/5/2017
61	Kim Nam Ung	Mwakilishi wa Benki ya Kimataifa ya Ilsim huko Mosko, Urusi	Korea Kaskazini	8/5/2017
62	Pak Il Kyu	Mwakilishi wa Shirika la Jumla la Ryonbong nchini Uchina	Korea Kaskazini	8/5/2017

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Watu Binafsi				
#	Jina	Uhusiano	Uraia	Tarehe ya Kuorodheshwa
67	Kim Kyong Il	Mwakilishi wa Naibu wa Chifu wa Benki ya Biashara ya Nje nchini Libya	Korea Kaskazini	2017-12-22
68	Kim Tong Chol	Mwakilishi wa Benki ya Biashara ya Nje huko Shenyang, Uchina	Korea Kaskazini	2017-12-22
69	Ko Chol Man	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Biashara ya Nje	Korea Kaskazini	2017-12-22
70	Ku Ja Hyong	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Biashara ya Nje	Korea Kaskazini	2017-12-22
71	Kyong Hwan	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya East Land	Korea Kaskazini	2017-12-22
72	Pae Won Uk	Mwakilishi wa Benki ya Daesong huko Beijing, Uchina	Korea Kaskazini	2017-12-22
73	Pak Bong Nam	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Kimataifa ya Ilsim	Korea Kaskazini	2017-12-22
74	Ri Chun Hwan	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Biashara ya Nje	Korea Kaskazini	2017-12-22
75	Ri Chun Song	Mwakilishi wa ng'ambo wa Benki ya Biashara ya Nje	Korea Kaskazini	2017-12-22
77	Ri Song Hyok	Mwakilishi wa Kampuni ya Kuendeleza Mikopo ya Koryo na Benki ya Koryo nchini Uchina	Korea Kaskazini	2017-12-22
78	Ri U'n-So'ng	Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Muungano wa Korea (KUDB) huko Mosko, Urusi	Korea Kaskazini	2017-12-22

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Mashirika			
#	Shirika	Uhusiano (mmiliki, kampuni ifichayo, mshiriki, inamilikiwa/kuendeshwa na, n.k.)	Tarehe ya Kuorodheshwa
1	Shirika la Biashara za Kuendeleza Uchimbaji Madini la Korea (KOMID)	Kamati ya Pili ya Uchumi	4/24/2009
2	Shirika la Jumla la Korea Ryonbong		4/24/2009
3	Banki ya Kibiashara ya Tanchon	Kamati ya Pili ya Uchumi, KOMID	4/24/2009
4	Kampuni ya Biashara ya Namchongang	Ofisi ya Kuu ya Nishati ya Nyuklia (GBAE)	7/16/2009
5	Kampuni ya Kielektroniki ya Hong Kong	Banki ya Kibiashara ya Tanchon na KOMID	7/16/2009
7	Ofisi ya Kuu ya Nishati ya Nyuklia (GBAE)	Serikali, Kampuni ya Biashara ya Korea Kumsan, Kampuni ya Biashara ya Namchongang	7/16/2009
13	Benki ya East Land	Benki ya Dongbang, Tongbang U'nhaeng, na Benki ya Tongbang	1/22/2013
14	Kampuni ya Biashara ya Korea Kumryong	KOMID	1/22/2013
16	Shirika la Mradi wa Pamoja la Mashine la Korea Ryonha	Shirika la Jumla la Korea Ryonbong	1/22/2013
17	Shirika la Kimataifa la Leader (Hong Kong)	KOMID	1/22/2013
21	Chuo cha Sayansi cha Ulinzi wa Nchi (ANDS)	Chuo cha Pili cha Sayansi Asilia	3/2/2016
39	Kampuni ya Kimtaifa ya Korea ya Mradi wa Pamoja wa Kemikali (KICJVC)	Shirika la Jumla la Korea Ryonbong	11/30/2016
44	Shirika la Biashara la Korea Kumsan	GBAE	2017-06-02
50	Kundi la Kampuni la Miradi ya Nje ya Mansudae	Chama cha Wafanyakazi cha Korea	8/5/2017

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Mashirika			
#	Shirika	Uhusiano (mmiliki, kampuni ifichayo, mshiriki, inamilikiwa/kuendeshwa na, n.k.)	Tarehe ya Kuorodheshwa
55	Kampuni ya Usafirishaji na Teknolojia ya Chang An	Mmiliki aliyesajiliwa, meneja wa meli, na meneja wa biashara wa HUA FU yenye bendera ya Panama	2018-03-30
56	Kampuni ya Usafirishaji ya Chonmyong	Mmiliki aliyesajiliwa wa CHON MYONG 1 yenye bendera ya Korea Kaskazini	2018-03-30
58	Kampuni ya Usafirishaji ya Hapjanggang	Mmiliki aliyesajiliwa na tanka la Korea Kaskazini la NAM SAN 8	2018-03-30
59	Huaxin Shipping Hongkong Ltd	Meneja wa biashara na meli wa ASIA BRIDGE 1 inayomilikiwa na Hong Kong	2018-03-30
61	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Achim	Mmiliki aliyesajiliwa wa CHON MA SAN yenye bendera ya Korea Kaskazini	2018-03-30
62	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Ansan	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la AN SAN 1	2018-03-30
63	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Myongdok	Mmiliki aliyesajiliwa wa YU HYONG 5.	2018-03-30
64	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Samjong	Mmiliki aliyesajiliwa wa matanka ya Korea Kaskazini ya SAM JONG 1 na SAM JONG 2	2018-03-30
65	Kampuni ya Usafirishaji ya Korea Samma	Mmiliki wa SAM MA 2 yenye bendera ya Korea Kaskazini	2018-03-30
66	Korea Yujong Shipping Co Ltd	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la YU JONG 2	2018-03-30
67	Kampuni ya Koti	Meneja wa meli na meneja wa biashara wa KOTI yenye bendera ya Panama	2018-03-30
68	Kampuni ya Usafirishaji ya Myohyang	Meneja wa meli wa tanka la YU SON la Korea Kaskazini	2018-03-30
69	Kampuni ya Usafirishaji ya Paekma	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la PAEK MA	2018-03-30
70	Kampuni ya Usafirishaji Baharini ya Phyongchon	Mmiliki aliyesajiliwa wa tanka la Korea Kaskazini la JI SONG 6	2018-03-30

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

Mashirika			
#	**Shirika**	**Uhusiano (mmiliki, kampuni ifichayo, mshiriki, inamilikiwa/kuendeshwa na, n.k.)**	**Tarehe ya Kuorodheshwa**
72	Shanghai Dongfeng Shipping Co Ltd	Mmiliki aliyesajiliwa, msimamizi wa biashara na meli wa DONG FENG 6	2018-03-30
73	Kampuni ya Usafirishaji Kimataifa ya Shen Zhong	Meneja wa biashara na meli wa HAO FAN 2 na HAO FAN 6 zenye bendera ya St Kitts-Nevis	2018-03-30
74	Kampuni ya Kusafirisha Mizigo Ulimwenguni ya Weihai	Meneja wa biashara na meli ni XIN GUANG HAI	2018-03-30

Shawna Meister - Mchangiaji Mkuu wa CCSI

Mchambuzi wa sera na utafiti, Shawna Meister amefanya kazi na CCSI tangu ilipanzishwa kwenye miradi anuwai kwa miaka minane iliyopita. Historia yake inajumuisha kuchambua kazi ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa kwenye juhudi za jumla za kusuluhisha vita, vita vya wenyewe kwa wenyewe barani Afrika na kwenye Mashariki ya Kati, changamoto za kutekeleza sheria za vikwazo vya kupinga usambazaji. Hivi karibuni, kama sehemu ya jitihada ya utafiti wa kuainisha ya CCSI, Shawna ameongoza uchambuzi wa sifa na shughuli za watu binafsi na mashirika yaliyoorodheshwa ili kutambua ruwaza na uhusiano ndani ya na kwenye mifumo ya vikwazo. Ameandika machapisho kadhaa yakiwemo kuandika ripoti za kiufundi na kichambuzi, uchunguzi wa kifani, makala ya majarida, na amechangia kwenye miongozo ya kupinga usambazaji na vitavu vyote ambavyo vimechapishwa na CCSI. Uhodari wa Shawna unajumuisha usimamizi wa miradi ya utafiti yenye daraja anuwai na kugeuza uchambuzi na maelezo tata yawe bidhaa zinazoweza kutumika kama vile miongozo ya mafunzo, miongozo ya kielimu, rasilimali na vifaa vya umma, na tovuti.

Enrico Carisch www.comcapint.com
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

Loraine Rickard-Martin
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com